



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE



Unapojibu tafadhali taja:-

Kumb. Na. NDC/I.20/6/VOL.VII/146

25/05/2022

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe anatangaza **nafasi nne (4) za dereva daraja la II pamoja na nafasi tatu (3) za katibu Mahsusi daraja la III** hivyo anakaribisha maombi kwa watanzania wote wenye sifa na uwezo, kwa ajili ya kujaza nafasi ya kazi kama ilivyo orodheshwa katika tangazo hili. Aidha mnajulishwa kuwa mwisho wa maombi haya ni tarehe **07/06/2022**.

1. Dereva Daraja II - NAFASI 4

1.1 Sifa za mwombaji.

- Mwenye elimu ya kidato cha nne (IV) au sita (VI)
- Awe na Leseni daraja E au C₁
- Awe na Cheti cha Mafunzo ya Msingi (Basic Driving Course) kinachotolewa na Chuo cha Mafunzi ya Ufundi Stadi (VETA) au Chuo kingine chochote kinachotambulika na Serikali. Aidha, kwa mwombaji mwenye cheti cha mafunzo daraja la II atafikiriwa kwanza.

1.2. MAJUKUMU

- Kufanya Ukaguzi wa gari kabla na baada ya safari ili kubaini usalama wa gari
- Kuwapeleka Watumishi sehemu mbalimbali
- Kufanya Matengenezo Madogo Madogo ya gari.
- Kukusanya na Kusambaza Nyaraka mbalimbali
- Kujaza na kutunza taarifa mbalimbali za safari kwenye daftari la safari (Log Book)
- Kufanya Usafi wa gari.

MSHAHARA

- Kwa kuzingatia Muundo na Ngazi za Mshahara ya Watumishi wa Serikali yaani **TGS B₁ kwa mwezi**.

2. KATIBU MAHSUSI Daraja III - NAFASI 3

2.1 Sifa za mwombaji.

- d) Mwenye elimu ya kidato cha nne au sita
- e) Awe na Astashahada(NTA Lever 5) ya Mafunzo ya Uhazili na kufaulu Mtihani wa hatua ya Tatu.
- f) Awe amefaulu somo la Hati Mkato ya Kiswahili na Kingereza Maneno 80 kwa dakika moja na awe amepatamafunzo yakomputa kutoka chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC) au chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali.

2.1 MAJUKUMU

- a) Kuchapa Barua,taarifa na nyaraka mbalimbali
- b) Kusaidia kupokea wageni na kuwasaili shida zao na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa.
- c) Kusaidia kutunza Taarifa/Kumbukumbu za Matukio,Miadi,Wageni Tarehe za Vikao, Safari za Wakuu wake na ratiba ya Kazi zingine.
- d) Kusaidia kutafuta na kumpatia Mkuu wake Majalada, nyaraka au kitu chochote kinachohitajika katika shughuli za kazi hapo Ofisini.
- e) Kusaidia kupokea majalada kuyagawa kwa maafisa walio katika sehemu alipo, kuyatunza na kuyarudisha sehemu zinazohusika

MSHAHARA

- a). Kwa kuzingatia Muundo na Ngazi za Mshahara ya Watumishi wa Serikali yaani **TGS B₁ kwa Mwezi**

3. MAELEKEZO YA UJUMLA

- i. Waombaji wote wawe raia wa Tanzania ambao hawazidi umri zaidi ya miaka 45 na hawapungui umri wa miaka 18.
- ii. Waombaji wote waombe kwa kufuata masharti ya TANGAZO LA KAZI,
- iii. Waombaji lazima waambatanishe nakala za vyeti vifuatavyo:-
 - a) Cheti cha mtihani wa kidato cha nne au sita.
 - b) Cheti cha kuzaliwa.
 - c) Picha mbili za passport size.
 - d) Nakala ya Kitambulisho cha NIDA
- iv. Hati ya matokeo ya kidato cha nne/sita (Result slip) haitafanyiwa kazi.
- v. Barua ya maombi iandikwe kwa Kiswahili au kingereza.

- vi. Watakaoitwa kwenye usaili watajigharamia wenyewe.
- vii. Tarehe ya mwisho ya kupokea maombi ni tarehe 07/06/2022 saa 9:30 alasiri, baada ya tarehe hiyo kupita maombi hayatapokelewa na watakao chaguliwa kufanya usaili watajulishwa tarehe ya usaili kupitia tovuti ya Halmashauri www.njombedc.go.tz na kwenye mbao za matangazo za Halmashauri.

Barua zote zitumwe kwa:-

MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE,
S.L.P 547,
NJOMBE.

Tangazo hili limetolewa na:-



Sharifa Y. Nabalang'anya
MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE